- Matamvua - Yenye unyevunyevu, yanayong'aa, yenye rangi ya waridi (pinki) au nyekundu
- Tumbo - Halijavimba, halijalegea na limekaza
- Eneo la kutolea Uchafu/Kinyesi – Umefunga
- Utumbo - Laini, safi unaong'aa, hauna uteute mzito unaoteleza
- Uti wa Mgongo - Minofu imeshikamana vizuri na uti wa mgongo

**Samaki Aliyeharibika:**

- Harufu - Haipendezi, yenye reha ya asidi na harufu kama ya hewa ya amonia,
- Muonekano - Rangi iliyofifia na isiyong'aa
- Uimara wa minofu - Mwili laini, ukibonyeza alama inabaki imebonyea
- Uvujaji/Mnyeso - Samaki mwenye unyevunyevu unaonata
- Magamba - Yanatoka kwa urahisi Ina mikunjo,
- Ngozi - imepoteza rangi ya asili na ni rahisi kuachia
- Macho - Yasiyo mang'avu na mboni yenye mtoto na yamebonyea ndani
- Funiko la Mashavu/Matanvua Limejiachia na lina matone ya damu
- Matanvua – Kavu,kahawia, yasiong'aa
- Tumbo - Halijavimba, halijalegea na limekaza
- Eneo la kutolea Uchafu/Kinyesi - Umefunga
- Utumbo - Laini, safi unaong'aa, hauna uteute mzito unaoteleza
- Uti wa mgongo - Minofu imeshikamana vizuri na uti wa mgongo
- Minofu - Imara, laini na inanyumbuka
- Yenye unyevunyevu, yanayong'aa, yenye rangi ya waridi (pinki) au nyekundu
- Halijavimba, halijalegea na limekaza

*Manufaa ya kuzingatia mbinu bora za uhudumiaji wa Samaki na mazao yake*


Kwa Maelezo Zaidi Wasiliana na:

**AFISA MFAWIDHI WA KANDA**

**NA MSIMAMIZI WA MRADI (TASP II)**

KITENGO CHA KUTHIBITI UBORA WA SAMAKI

NA VIWANGO KANDA YA ZIWA VICTORIA

S.L.P. 1213 MWANZA

**SIMU**

+255 28 2550864

+255 754/784 437234

**Barua Pepe:** nfqcl_mz@yahoo.co.uk

**Tovuti:** www.nfqcl.go.tz


## JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

## WIZARA YA MAENDELEO YA MIFUGO NA UVUVI

IDARA YA MAENDELEO YA UVUVI
KITENGO CHA KUTHIBITI UBORA WA SAMAKI NA VIWANGO



# Mbinu bora za uhudumiaji wa Samaki na mazao yake

TRADE AND AGRICULTURE SUPPORT PROGRAMME II (TASP II)

*Imetayarishwa na Maabara ya Kitaifa ya Samaki chini ya Mpango wa TASP II kwa ufadhili wa mfuko wa Maendeleo ya Jumuiya ya Ulaya (EDF)*

# Mbinu bora za uhudumiaji wa Samaki na mazao yake



*Kimetayarishwa na NFQCL – Nyegezi, kupitia Mpango wa TASP II kwa Ufadhili Mfuko wa Maendeleo wa Jumuiya ya Ulaya (EDF).*

### *Utangulizi*

Uhudumiaji Bora wa Samaki na mazao yaje ni ile hali ya kuvua, kukusanya, kusafirisha, kupokea, kuhifadhi na kuchakata samaki katika mazingira yasiyosababisha kuharibika kwa samaki. Samaki anaweza kuharibika kutokana na uhudumiaji usiozingatia Kanuni za Usafi na Usalama.

### *Usafi Binafsi wa Wahudumiaji wa Samaki*

- Anatakiwa kuoga kwa sabuni kabla ya kwenda mavuvini au kuhudumia samaki
- Mvuvi anatakiwa asiwe mgonjwa na wala asiwe na magonjwa ya kuambukiza.
- Mvuvi anatakiwa kuvaa sare wakati wote wa kazi
- Asiwe na tabia ya kuvuta sigara, kutema mate ovyo wakati wa kuhudumia samaki

### *Usafi wa Vyombo na zana za uvuvi*

- **Chombo cha kuvulia/kukusanyia samaki**
  a. Kinatakiwa kusafishwa kabla na baada ya kutoka mavuvini kwa maji safi na salama.
  b. Kiwe na sehemu maalum ya kutosha na safi ya kuhifadhia samaki inayozuia joto.
  c. Maji ya Ngama ya boti yanapaswa kuondolewa mara kwa mara.
  d. Kiwe na sehemu maalum ya kuhifadhi zana na mafuta.
- **Zana za kuvulia samaki**
  a. zinapaswa kusafishwa kabla ya kupelekwa mavuvini.
  b. Zinasafishwa kwa maji safi na salama
  c. Zinatakiwa kukaguliwa na kukarabatiwa mara kwa mara

### *Uhifadhi na Matumizi bora ya barafu*

- Barafu utengenezwa kwa maji safi na salama
- Kuhifadhiwa vyema katika chombo chenye kutunza ubaridi
- Uwiano wa barafu na samaki ni 1:1
- Barafu ya chengachenga ni bora zaidi
- Barafu itumike mara moja tu

### *Usafi na utunzaji wa Mwalo rasmi wa kupokelea samaki*

- Uwekwe uzio kuzuia wanyama na watu wasiohusika kuingia,
- Kuwepo na banda lenye kivuli
- Kuwepo na mfumo wa maji safi na maji taka
- Kuwe na choo na bafu
- Kuwe na vyumba vya kuhifadhia zana za uvuvi, matengenezo ya zana za uvuvi, vifaa vya usafi na ofisi za kazi,
- Kiwe na eneo maalumu la kuegesha magari na mitumbwi
- Kuwe na utaratibu wa mara kwa mara wa ukaguzi na marekebisho na mapungufu yanayobainika

### *Utambuzi wa samaki Bora na Aliyeharibika*

**Samaki Bora:**

- Harufu - asilia yenye reha ya magugu ya ziwani
- Muonekano - Ananga'aa, rangi inaonekana vizuri, hakuna matone ya damu kichwani na uti wa mgongo
- Macho - Mang'avu, yasiyobonyea na mboni zinazong'aa
- Magamba - Yanang'aa na yamejishikiza imara
- Uimara wa Minofu - Imara isiyopindika, kakamavu, inayorudi ikibonyezwa
- Uvujaji/Mnyeso - Samaki mwenye unyevunyevu ambao unaonyesha kama maji
- Ngozi - Imekaza na imeshikiza kwa uimara
- Funiko la Mashavu/Matamvua - Limejishikiza imara na halina matone ya damu